## Ernest Bernard Phillips, (1892-1977)

Ernest Bernard Phillips, mwinjilisti na mwalimu, alizaliwa huko Stroud, Kent, mnamo Novemba 20, 1892, mtoto wa mwisho wa watoto 10. Baba yake alikuwa sajenti mkuu katika Jeshi la Wanamaji la Kifalme.

Phillips, pamoja na washiriki kadhaa wa familia yake, akawa Madventista Msabato, na mwaka wa 1907 alikwenda Chuo cha Mafunzo ya Wamishonari cha Stanborough Park na kumaliza kozi yake ya theolojia. Ingawa alikuwa kijana tu, alichukua mfululizo wa masomo ya Biblia huko Chatham, alikokuwa anasoma ambako aliongolewa na kukubali kuwa mchungaji na akaenda kusoma katika Chuo cha Stanborough, ambako hatimaye akahitimu na kuwa mchungaji rasmi aliyewekewa mikono.

Mnamo 1912 Phillips aliitikia mwito wa huduma ya misheni, alihudhuria kozi fupi ya matibabu ya kitropiki katika Chuo cha Livingstone, na akiwa na umri wa miaka 19 alisafiri kwa meli ya SS Field Marshall hadi Mombasa. Alianza huduma yake katika Koloni la Kenya, Afrika Mashariki, akifanya kazi Kisumu, Gendia, na Weary Hill. Alianzisha kituo cha Misheni cha Karunga kwenye Ziwa Victoria ambacho, kwa sababu ya hali mbaya ya afya, kilifungwa, majengo yakavunjwa, na nyenzo zilizobaki zilizotumika kujenga Misheni ya Kanyadota. Muda mwingi alifanya kazi peke yake, na baadaye alisema kwamba hata aliwaonea wivu watu gerezani, kwa sababu angalau walikuwa na mtu wa kuzungumza nao. Hata hivyo, alijifunza Kiswahili na Kijaluo, akapata ufasaha katika kila lugha, na kutafsiri sehemu nyingi za Agano Jipya katika lugha hizi za kienyeji.

Wakati wa Vita vya Kwanza vya dunia, wakati Wajerumani walipovamia Nyanza Kusini, wamishonari wa Kiingereza walihamishwa hadi kambi karibu na Kituo cha Kaimosi cha Jumuiya ya Marafiki, sio mbali na Kisumu. Baada ya vita vituo vingi vya misheni vilikuwa vimeporwa na kuharibiwa, na kulikuwa na kazi kubwa ya kujenga upya. Phillips alishiriki katika ufyatuaji wa matofali, useremala, na kutengeneza makabati huku akisaidia kujenga upya hospitali. Mnamo 1917 alifanya kazi Kamagambo, kituo cha misheni, kama maili 40 ndani ya bara, kusini-mashariki mwa Gendia, ambapo watu 37 walibatizwa.

### Ndoa

Phillips alifika nyumbani kwenye hafla yake ya kwanza mnamo 1920, na kuhitimu kutoka kwa kozi ya uchungaji katika Chuo cha Stanborough. Alifanya mikutano ya injili huko Cambridge, na alikutana na mwanamke mchanga ambaye alikuwa akiandikiana naye, Lily Hugill, mwanafunzi katika Chuo cha Stanborough. Mnamo Juni 22, 1921, walioa, na mnamo Desemba 18 mwaka huo walisafiri kwa meli kutoka Southampton hadi Mombasa kuanza huduma ya misheni pamoja.

Waliteuliwa kuanzisha tena kituo cha Busegwe huko Tanganyika (katika Tanzania ya sasa), na kufanya kazi huko kwa miaka kadhaa. Binti yao, Joyce alizaliwa mwaka wa

1923, na mwaka wa 1925 mtoto wao wa kiume, Bernard. Ernest mara nyingi hakuwa anakaa nyumbani, mara nyingi alikuwa akifanya safari tena kwa miguu, akiwatembelea watu na kuwahubiri. Umeme ulikuwa mgumu kupata nyakati hizo, barua kutoka na kwenda Uingereza zilichukua muda mrefu, na walipata hisia kali ya kutengwa. Hata hivyo, wengi walibatizwa na kujiunga na kanisa la Busegwe, na mwaka wa 1926 Ernest alitawazwa kwa huduma ya injili akiwekewa mikono ya uchungaji huko Gendia, Kenya, na W. W, Armstrong.

Familia ya Phillips ilirudi nyumbani kwao Uingereza mnamo 1927 na kukaa na wazazi wa Ernest huko Kent. Wakiwa Uingereza, mtoto wao Bernard alikufa katika ajali. Alizikwa huko Gillingham, na familia iliyofiwa ilirudi tena katika utume zaidi Tanganyika, ambapo Ernest alikuwa msimamizi wa kituo cha Misheni cha Mwagala.

Tanganyika ilikuwa eneo gumu kwa sababu ya hali ya hewa na hali ya kutengwa kutokana na kukosa mawasiliano na miundo mbinu mibovu. Hata hivyo, familia ya Phillips ilibakia huko kuanzia 1927 hadi 1931. Majirani zao wa karibu Waingereza walikuwa Harry na Ada Robson, ambao walikuwa kwenye Kituo cha Ntusu maili nyingi sana. Mnamo 1928, binti wa pili, Rachel, alizaliwa na Ernest na Lily katika hospitali ya Kendu nchini Kenya, ambayo ilikuwa imefunguliwa mwaka wa 1925 na Dk GAS Madgwick.

**Tatizo la maji**

Phillips alitengeneza samani nyingi katika nyumba yao rahisi. Walikabiliwa na matatizo ya mara kwa mara ya kupata chakula kinachofaa kwa mtoto na maji ya kunywa kwa ajili ya familia. Walifua nguo katika maji ya mto, kwani maji ya kunywa yaliyotolewa kutoka kwa tanki la maji ya galoni 400 yalikuwa ya thamani sana kutumika kwa kuosha. Kwa kweli, Ernest aliomba kwa bodi ya Misheni kwa ajili ya tanki la ziada la bati, lakini hakukuwa na fedha.

Tatizo lao lilikuwa kwamba wakati tanki la maji lilikuwa limejaa, wakati wa msimu wa mvua, shinikizo kubwa la maji lilisababisha uvujaji wa tanki hilo, na kutengeneza chemichemi ya maji yanayovuja. Wakati mmoja Phillips alishusha tanki moja chini mara tatu ili kurekebisha uvujaji ambao ulikuwa mgumu kuutatua. “Lakini Bwana alikuwa akitubariki sana licha ya ugumu wa kupata vifaa nk”, Lily Phillips aliandika. Lily aliwafundisha wanawake wenyeji kanuni na desturi za kujitunza wao wenyewe, nyumba zao, na familia zao vyema.

Ugumu mkubwa zaidi wa mawasiliano uliowafanya wajisikie kutengwa ulikuwa ukijitokeza wakati daktari alipohitaji kwenda kumuhudumia mgonjwa. Mwishoni mwa 1930, Lily Phillips aliugua homa ya blackwater. Familia ya akina Phillips walikuwa wamepanga kurejea Uingereza kwa ajili ya kumsomesha Joyce, kwani alikuwa na umri wa karibu miaka minane, na hakukuwa na elimu ya Uingereza iliyokuwa inapatikana katika sehemu hiyo ya Tanganyika kwa watoto wa umri huo. Lily alikuwa anaumwa sana hata hakuweza kutembea wala kukaa, hivyo siti ya nyuma ya gari la

Robson ilitolewa na kuwekwa magunia yaliyojaa mchanga ili alale. Safari ya kwenda hospitali ya karibu ilichukua siku mbili, kupitia mito iliyojaa na barabara mbovu. Ingawa walifika hospitali yenye huduma kama zile zipatikanazo Ulaya huko Mwanza, Januari 28, 1931, Lily Phillips alifariki na kuzikwa huko katika sehemu ya makaburi ya Waingereza.

Ernest Phillips na binti zake walikaa na akina Robson kwa majuma kadhaa huku mali zao chache zikiwa zinafungwa kwa ajili ya kusafirishwa, kisha wakarudi Uingereza, ambako walikaa kwa muda nyumbani kwa wazazi wa Ernest kwenye Mtaa wa Canterbury huko Gillingham.

Muda fulani baadaye, Mkuu wa WGC Murdoch alimteua Phillips kufundisha katika Chuo cha Wamishonari cha Newbold. Kuanzia 1931 hadi 1957 alitoa huduma isiyokatika katika huko. Mnamo 1933 alifunga ndoa na Alice Gordon, mfanyakazi wa Biblia kutoka Glasgow. Binti yao Clemency alizaliwa mwaka wa 1936.

Alipokuwa akifundisha Newbold, Phillips alianza kozi ya kina ya masomo kwa mawasiliano katika Chuo Kikuu cha London. Alipata shahada ya kwanza mwaka wa 1936, Shahada ya Uzamili ya Theolojia mwaka wa 1939, na Diploma ya Elimu kutoka Chuo Kikuu cha Oxford mwaka wa 1941. Alikuwa Muadventista wa kwanza wa Sabato nchini Uingereza kupata digrii za juu za theolojia. Alifundisha masomo mengi katika Chuo cha Newbold yakiwemo Kigiriki cha Agano Jipya, Kiebrania, Saikolojia, Historia ya Kanisa, Historia ya Kiingereza, Uchunguzi wa Biblia, Nyaraka, na Mafundisho ya Biblia. Alijulikana kwa upendo miongoni mwa wanafunzi wake wa Kigiriki kama "Philippos," na alisifiwa kwa ucheshi wake, fadhili zake, na kujali kwake wanafunzi wake wote.

Wakati wa miezi mitatu ya kiangazi iliyofuatana, huku akiwa hafundishi wanafunzi, Phillips aliendesha mikutano ya kiinjilisti huko Hull, Leeds, na Sheffield.

Baada ya miaka 26 ya utumishi katika Chuo cha Newbold, Phillips aliitwa kuhudumu katika Misheni ya Ireland, na kisha Uingereza Kaskazini. Hatimaye alistaafu katika kijiji cha Binfield mwaka wa 1963, ambako aliendelea kuandika makala kwa gazeti la Our Times, na kuziuza nyingi ya nakala zake kwa watu wa kijiji hicho. Alifundisha madarasa ya Kigiriki, akawashauri na kuwahudumia wanafunzi waliofunga ndoa chuoni, na kufanya mafunzo ya Biblia na mikutano ya maombi nyumbani kwake mwenyewe.

Wakati fulani aliulizwa na mkwe wake, “Umejitolea sana maishani mwako. Je, utafanya vivyo hivyo tena?” Alijibu kwa urahisi, “Ninawezaje kumwambia Mwokozi wangu tunapokutana, kwamba nimetoa dhabihu kwa ajili Yake wakati hazilingani na yote ambayo amenifanyia?”

Ernest Phillips alikufa baada ya kuugua kwa muda mfupi mnamo Juni 4, 1977.